Maswali

1. Nani alifanya Sulemani awe na hekima na mali?
2. Malkia wa Sheba alisikia habari ya Sulemani namna gani?
3. Mbona Malkia wa Sheba alienda kumwona Sulemani?
4. Sulemani aliweza kujibu maswali ya Malkia wa Sheba yote?
5. Sulemani alionyesha Malkia nini?
6. Sulemani alifanyia Malkia karamu. Eleza juu ya karamu.
7. Malkia wa Sheba, zaidi alitaka ajionee nini?
8. Hadithi juu ya Sulemani iliongezwa sifa?
9. Sulemani alipea Malkia wa Sheba nini?
10. Nini ilishangaza Malkia wa Sheba?

Majibu

1. Mungu alimfanya Sulemani awe na hekima na mali.
2. Wafanyi biashara walimwambia habari ya Sulemani.
3. Alitaka kujua kama hadithi juu ya Sulemani ilikuwa ya kweli.
4. Ndiyo, Sulemani aliweza kujibu maswali ya Malkia wa Sheba yote.
5. Majengo ya ajabu. Mali na utukufu ya ufalme wake.
6. Watumishi wengi. Vyakula vingi vilivyo tofauti tofauti. Sahani za dhahabu.
7. Mungu mwenye Sulemani aliabudu.
8. La.Sulemani alikuwa na hekima na mali kuliko vile aliambiwa.
9. Zawadi nyingi. Kila kitu alichotaka.
10. Baraka za hekima na mali yenye Mungu alikuwa amempa Sulemani.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 2 Mwaka wa 2

67 Malkia wa Sheba

Kwa Biblia

1 Wafalme 10:1—25

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu alibariki Sulemani kwa hekima na mali nyingi. Mataifa yote yaliyokaribu yalisikia kwamba Mungu alikuwa amebariki Sulemani

Somo

Kwa somo lililopita tulisoma kwamba Mungu alikuwa amebariki Sulemani kwa hekima na mali. Sulemani alikuwa wa hekima sana. Tena alikuwa Mfalme tajiri sana. Mfalme Sulemani alikuwa ndiye Mfalme tajiri zaidi kuliko wafalme wote ulimwenguni. Alifanya biashara na wafalme wa Misri, Syria na Tiro. Manowari za biashara zilienda Ofiri (labda ndiyo Hindi au India) kila baada ya miaka tatu na kuleta mali nyingi. Meli zake zilileta dhahabu, fedha, pembe, nyani na tausi. Sulemani alitawala juu ya wafalme wengi. Walilipa dhahabu na fedha nyingi kama kodi.



Wafanyi biashara wa Sulemani walisafiri nchi nyingi. Walizuru mataifa mengi. Popote walipoenda waliambia watu juu ya mali ya Sulemani na hekima yake kuu. Wafalme wengi walikuja kuona Sulemani na kusikia hekima zake. Wafanyi biashara wa Sulemani walienda nchi ya Sheba kufanya biashara ya dhahabu na manukato.

Wafanyi biashara waliambia malkia wa Sheba hadithi nyingi juu ya Sulemani. Walimwambia juu ya hekima nyingi ya Sulemani. Walimwambia juu ya mali nyingi ya Sulemani. Walimwambia juu ya Mungu mkuu aliyekuwa amembariki Sulemani. Alidhania kwamba hadithi zingine lazima zimezidiwa sifa. Malkia wa Sheba aliamua kwenda kwa Sulemani ili aone kama hizo hadithi zote ni za kweli. Haja ya Malkia kubwa ilikuwa kuchunguza juu ya Mungu aliyeabudiwa na Sulemani.

Malkia wa Sheba alisafiri kwenda Yerusalemu. Alienda na kikundi kikubwa cha watu. Aliletea Mfalme Sulemani zawadi nyingi. Malkia wa Sheba aliletea Sulemani zawadi nyingi kama manukato, dhahabu nyingi na mawe mazuri. Alibebea kwa ngamia. Mfalme Sulemani alimkaribisha malkia wa Sheba.

Malkia wa Sheba alizungumza na Mfalme Sulemani juu ya mambo mengi sana. Alimuuliza maswali yote magumu na mafumbo yenye alikuwa amepanga kumjaribu nayo. Malkia wa Sheba alishangaa kuona Mfalme Sulemani anajibu maswali na kufumbua mafumbo magumu yote. Mfalme hakukuwa na shida ya kumueleza malkia jambo lolote.

Mfalme Sulemani alionyesha Malkia mali na utukufu wote wa ufalme wake. Aliona majengo kubwa na mzuri sana hapo Yerusalemu. Aliona Hekalu nzuri ya Mungu kwa mlima wa Moria.



Sulemani alimwonyesha jumba ya Mfalme pia iliyokuwa imejengwa kwa ustadi mzuri. Kulikuwa na ngazi ya ajabu iendayo kwa hilo jumba la Sulemani. Alikuwa na kiti cha enzi cha dhahabu. Vipandio vilikuwa vya dhahabu na kwa kila kipandio kulikuwa na simba wa dhahabu pande zote. Malkia wa Sheba aliona jumba ya Mfalme yenye Sulemani alijengea malkia wake. Ilikuwa na nguzo ya mierezi. Kulikuwa na bustani nzuri na viziwa pia. Labda alienda kuona mji mkubwa wa Sulemani na magari huko Megido. Kule Sulemani alijenga vipanda 40,000 vya farasi wake.

Mfalme Sulemani alifanyia Malkia wa Sheba karamu kubwa. Sulemani alikuwa na watumishi wengi sana. Meza zilijaa vyakula vingi vya kupendeza na vya aina tofauti. Sahani zote mezani zilikuwa za dhahabu. Malkia wa Sheba alikuwa na mshangao kwa kila alichoona.

Malkia wa Sheba alipendezwa na sadaka zenye Mfalme Sulemani alitolea Mungu kila siku. Aliona kwamba Mungu alibariki Sulemani kwa sababu ya maajabu yote aliyofanya.

Malkia wa Sheba aliambia Mfalme Sulemani kwamba alikuwa amesikia hadithi juu yake. Alifikiri hizo zote ziliongezewa sifa. Lakini sasa ameona hekima na mali yake. Alimwabia, hekima na mali yake iko zaidi na vile alisikia.

Sulemani alishukuru Malkia wa Sheba kwa zawadi zake. Sulemani pia alimpa Malkia wa Sheba zawadi nyingi. Alimpa kila kitu alichotaka. Baadaye Malkia aliondoka akaenda nyumbani. Alishangaa sana kwa sababu ya hekima na mali yenye Mungu alikuwa amempa Mfalme Sulemani.